JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

HOTUBA YA MHESHIMIWA MKUU WA MKOA WA IRINGA WAKATI AKIKABIDHI HATI MILIKI ZA ARDHI KATIKA HALMASHAURI YA MJI NJOMBE.

Mheshimiwa Anne Makinda (Mb) Mwenyekiti wa MKURABITA na Naibu Spika,

Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Njombe,

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Njombe,

Waheshimiwa Viongozi wa vyama vya Siasa, taasisi za dini na Mabenki,

Mratibu wa MKURABITA taifa,

Kamishna wa Ardhi Msaidizi Kanda ya Kusini Magharibi,

Mheshimiwa Diwani, Kata ya Njombe Mjini,

Wageni Wote Waalikwa Mabibi na Mabwana,

Asalam aleykum.

Kwanza napenda kuwashukuru sana wananchi wa Halmashauri ya Mji Njombe kwa kuitikia na kuukubali Mpango wa Urasimishaji wa Rasilimali Ardhi kufanyika katika Mji wenu nawapongeza sana. Naipongeza vile vile Ofisi ya RAIS – MKURABITA kwa kutekeleza kazi hii kwa ufanisi mkubwa kwa kushirikiana na Halmashauri yenu.

Ndugu wananchi,

Ardhi ndio mali pekee na ndio urithi wa aina yake ambao taifa la Tanzania linajivunia. Lakini Ardhi haiwezi kuwa na thamani kama haieleweki ipo wapi kwa maana ya kwamba haina anuani, ukubwa wake haueleweki, matumizi yake anayaelewa yule anayetumia ardhi pekee na pia umiliki wake haueleweki.

Wananchi wa Njombe mnao utajiri mkubwa sana wa Ardhi kwa kuwa ardhi yenu inafaa kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi. Katika Miji Ardhi inafaa sana kwa Makazi na Biashara, Vijijini Ardhi inafaa kwa Makazi, Kilimo cha mazao ya Chakula na Biashara na Ardhi isiyofaa kabisa kwa kilimo inafaa kwa upandaji miti ambao ni utajiri wa asili ambao wananchi wa Njombe mmejaliwa na Mwenyezi Mungu.

Ndugu wananchi,

Nafahamu kwamba ni wananchi wachache wanaofahamu umuhimu wa Kuandikishwa kwa Ardhi zao na wananchi wengi hukumbuka kuandikisha Ardhi zao mara wanapotakiwa kuitumia Ardhi katika masuala mbalimbali mfano, mtu anahitaji mkopo kutoka katika taasisi ya Fedha na kutakiwa kuwasilisha Hati Miliki ya Nyumba na inapotokea anakabiliwa na Mgogoro wa Ardhi.

Serikali inatambua kikamilifu kwamba Ardhi ndio chanzo kikubwa cha Mtaji wa Watanzania walio wengi na kinachotakiwa ni kuwasaidia wananchi hawa ili Ardhi yao ambayo ni sawa na Mtaji Mfu (Dead Capital) ifufuliwe na kuwa hai ili iweze kuwasaidia wananchi kama dhamana kwenye vyombo vya fedha, mahakamani LAKINI kubwa zaidi ni kuwa na dhamana ya uhakika yenye egemeo la Serikali (Goverment-backed security).

Ndugu wananchi,

Urasimishaji wa Ardhi na nyumba za Watanzania ni utekelezaji wa Ilani ya Chama tawala Sura ya Nne aya ya 42 (a) inayosema nanukuu:

Kuanza utekelezaji wa Mkakati wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania kwa lengo la kuwawezesha Watanzania kurasimisha Ardhi na nyumba zao ili waweze kuzitumia kupata mikopo ya Mabenki na mifuko mingine ya fedha inayokopesha. Aidha Mabenki nayo yataandaliwa ipasavyo katika kubadili tabia ili yaondokane na mawazo ya ugumu katika kutoa mikopo.

Ndugu wananchi,

Serikali tayari imefanya upande wake wa kufanikisha Urasimishaji wa Ardhi na Nyumba lakini haitaweza kumlazimisha mwananchi kuitumia Hati kwa namna yoyote ile halali inayoweza kumnufaisha ***"unaweza kumpelekea punda maji ya kunywa lakini huwezi kumlazimisha kuyanywa"*** Ndugu wananchi natoa wito itumieni Ardhi iwanufaishe.

Aidha Serikali kwa kutambua umuhimu wa kuendelea kuwasaidia wananchi wake, imeweka taratibu mbalimbali za kuweza kuwasaidia wananchi kupata mitaji kwa kutumia Ardhi katika taasisi za fedha Kwa:-

1. Kuanzisha mfuko wa kudhamini Mabenki na taasisi za fedha kwa ajili ya kuboresha utoaji wa mikopo kwa miradi midogo na ya kati (SME-CGS)

2. Kuanzisha mfuko wa uwezeshaji ili wajasiliamali waweze kujipatia mikopo yenye masharti nafuu kwa mmoja mmoja, Vikundi na SACCOS kupitia Benki za CRDB na NMB.

3. Pia kwa mwaka wa fedha 2010/2011 serikali imeandaa utaratibu mpya wa kukopesha wakulima kwa gharama nafuu kupitia Benki ya Rasilimali (TIB) ujulikanao kama "Agricultural Window"

4. Aidha serikali tayari ilikaa na taasisi za fedha na kufanya marekebisho ya Sheria ya Ardhi No. 4 ya mwaka 1999 hasa vifungu vilivyohusu mikopo kupunguza mlolongo na urasimu kwa wananchi wenye Ardhi zilizoandikishwa kukopeshwa kiurahisi kama taasisi ya fedha itakuwa imeridhia kukopesha.

Ndugu wananchi,

Napenda kusisitiza kwamba Hati hizi mtakazokabidhiwa ni nyaraka muhimu sana, tafadhali kama utaamua kuitunza ndani itunzwe vema ili isiharibiwe kama utakubaliwa na taasisi za fedha basi mkopo huo utumike kwa lengo lililokusudiwa sio kuanza shughuli nyingine isiyo na tija na ambayo hailengi katika kukuendeleza wewe wala jamii yako au taifa.

Hitimisho

Nimeambiwa kwamba bado kuna wananchi wachache ambao hawajaona umuhimu wa kwenda kujaza fomu za kumilikishwa Ardhi pale kwenye Ofisi za Idara ya Ardhi, wengine wamedanganywa kwamba Hati zinazotolewa sio halisi kwa kuwa mchakato wa utoaji unakwenda haraka sana na gharama za uchangiaji ni nafuu mno, wengine wanaogopa gharama wanaona 120,000/= wanayochangia sasa ni kubwa mno. Jiulize Ardhi yako imepanda thamani kiasi gani, jiulize kwa juhudi zako pekee lini ungepata Hati Miliki ya Ardhi maana wapo wananchi wanaoona kwa mara ya kwanza Hati miliki za Ardhi leo. Hivyo msirubuniwe nendeni mkachukue fomu za maombi ya kumilikishwa Ardhi na changieni gharama za urasimishaji ili huduma hii iwafikie na wenzenu wa mitaa mingine ambao wanaitamani sana huduma hii iwafikie.

Hao wanaowaambia kwamba Hati hizi sio halisi wana wivu hawataki wewe ufanikiwe kama walivyofanikiwa wao ***"Akili za kuambiwa changanya na za kwako"*** Ndugu wananchi nawahakikishieni kwamba mnaweza kujiletea maendeleo yenu binafsi na nchi kwa ujumla kwa kutumia Hati Miliki za Ardhi mnazopewa leo, na wale ambao hawajaanza utaratibu wa kuzipata waanze mara moja.

Ahsanteni kwa kunisikiliza!